

Jarida la _____ Toleo Na. 8
SAMIA TENA
07/09/2025 2025-2030



ASANTE IRINGA





RAIS SAMIA: TUTAHAKIKISHA TANZANIA TUNAFIKISHA MEGAWATI 8000 ZA UMEME

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atanza mchakato wa kujenga miundombinu ya umeme itakayoweza Tanzania kuongeza megawati za umeme kutoka elfu nne za sasa hadi elfu nane.

Rais Samia ameyasema hayo leo mjini Iringa alipokuwa anahutubia maelfu ya wafuasi wa Chama hicho kikongwe nchini na Afrika.

Amesema ataongeza megawati hizi kupitia umeme wa joto ardhi na upepo ambazo ni rasilimali muhimu ambapo Tanzania imebarikiwa kuwa nazo.

Amesisitiza kuwa, lengo ni kuwa na umeme wa uhakika na kutosha ili kukuza uchumi kupitia viwanda na mwingine kuuza nchi za nje ili kuliingizia taifa fedha za kigeni.





RAIS SAMIA KUJENGA SOKO LA MACHINGA IRINGA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, iwapo atachaguliwa tena atajenga soko kubwa la Machinga Iringa mjini.

Rais Samia ameyasema hayo leo Iringa mjini wakati akihutubia maelfu ya wanachama wa chama hicho.

Amesema soko hilo almaarufu 'Machinga complex' litajengwa katika stendi ya mabasi ya zamani Iringa mjini.

Amefafanua kwamba, lengo la kujengwa soko hilo ni kuhakikisha wafanyabiashara wadogo wadogo mkoani humo wanafanya biashara zao kwa amani na kuchangia uchumi wa taifa.



DKT. SAMIA: SERIKALI ITAENDELEA KULEA VYAMA VYA USHIRIKA

Mgombea urais Kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, akipata ridhaa ya kuchaguliwa kuongoza tena, serikali yake itaendelea kulea vyama vya ushirika kwa kuvipatia mikopo ili kuwahudumia wanachama wake.

Amesema hayo leo mjini Iringa wakati akihutubia maelfu ya wanachama wa Chama hicho waliofika kumsikiliza akijinadi na kunadi wagombea wa viti vya ubunge na udiwani.

Amesema watavisaidia vyama hivi kuwa na watendaji mahili na kuwajengea uwezo katika matumizi ya TEHAMA ili wakulima waone masoko ya mazao yao yanavyoendeshwa duniani.

Ameongeza baadhi ya vyama vya ushirika nchini kama kile cha Iringa kinachoitwa 'Iringa Farmers Cooperative Union' kimeshawezeshwa na kujengewa uwezo na sasa kimepata bilioni moja kutoka benki ya Kilimo kwa ajili ya kununua ruzuku na kuuza kwa wanaushirika.



RAIS SAMIA: WANA CCM VUNJENI MAKUNDI TWEENDE PAMOJA



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesisitiza tena kwa wana CCM kuvunja makundi kipindi hiki cha Uchaguzi.

Akiongea mjini Iringa leo mbele ya wafuasi wa chama hicho waliofurika kumsikiliza, Rais Samia amesema, uteuzi ndani ya chama kwa nafasi mbalimbali umeisha viongozi waliopatikana ndo wamepewa ridhaa ya kugombea na wengine walioshindwa waunge mkono walioshinda.

Amesema huo ndo utamaduni wa siku zote wa CCM kuvunja makundi na wanachama kwenda kwa pamoja.

Rais Samia amesisitiza hili pia katika maeneo mengine aliyopita kuwa bila umoja hakuna ushindi wa kishindo.





RAIS SAMIA: TUTAHAKIKISHA TANZANIA INAENDELEA KUWA KINARA WA UZALISHAJI WA MAHINDI AFRIKA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Sulu Hassan amesema, iwapo atapata ridhaa ya kuongoza tena ataendelea kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa mahindi barani Afrika.

Rais Samia ameyasema hayo leo mjini Iringa wakati akihutubia maelfu ya wanachama wa CCM waliofurika uwanja wa Samora kumsikiliza.

Rais Samia ameeleza kuwa, mwaka huu Tanzania imekuwa ya pili Afrika kwa uzalishaji wa mahindi hivyo basi, atahakikisha anatoa pembejeo na ruzuku za kilimo ili watanzania waendeele kuzalisha kwa wingi na kukuza uchumi wa nchi.





DKT. SAMIA: TUTAANZISHA VITUO VYA UKODISHAJI WA ZANA ZA KILIMO NCHINI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine serikali yake itaanzisha vituo vya kukodisha zana za kilimo ili kusaidia wakulima kupata huduma hiyo kwa urahisi na bei nafuu.

Rais Samia ameyasema leo wakati akihutubia maelfu ya wanaCCM waliofurika kwa wingi kumsikiliza Iringa mjini.

Amesema atashirikiana na sekta binafsi kuanzisha vituo hivyo ili sekta hiyo iweze kuwahudumia wakulima zana hizo kwa bei nafuu.



SHILOLE, MADEE WASHUSHA VIBE IRINGA



CCM NI CHAMA KINACHOJALI WANANCHI WAKE





RAIS SAMIA KUWASHA UMEME MITAA 192 IRINGA MJINI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahakikisha mitaa yote 192 ya Iringa inawashwa umeme.

Rais Samia ameyasema hayo leo mjini Iringa wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofika kumsikiliza.

Rais Samia amesema tayari mitaa 189 kati ya 192 imewashwa umeme hivyo akichaguliwa kipindi cha pili atamalizia michache iliyobaki.

Amesema lengo ni kuhakikisha kila mtanzania anapata umeme wa uhakika ambao ni hitaji la msingi.





DK. NCHIMBI KUZISAKA KURA ZA CCM MKOA WA KAGERA

MGOMBEA Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, leo Septemba 7, 2025, ameruka kwa helikopta akizisaka kura za kishindo za CCM kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Balozi Dk. Nchimbi ameanza ziara yake ya kampeni Mkoani Kagera kwa kishindo, ambapo atafanya mikutano katika maeneo ya Ngara, Kyerwa, Katoro-Bukoba Vijijini na kuhitimisha kwa mkutano mkubwa Bukoba Mjini.

Katika mikutano hiyo, Dk. Nchimbi atanadi sera na Ilani ya CCM, akieleza mikakati na mipango ya chama hicho endapo kitapewa ridhaa ya kuongoza kwa miaka mitano ijayo.





KIGAE AMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUTEKELEZA ILANI YA CCM

Mgombe ubunge jimbo la Mufindi Kaskazini kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Mhe. Exaud Kigahe, amesema historia iliyowekwa na Rais Samia, kwa aliyotekeleza jimbo la Mufindi Kaskazini ni deni kwao nakuwasihi wananchi wa jimbo hilo kumlipa Oktoba 29, 2025.

Mhe. Kigahe, amesema hayo katika Mkutano wa Kampeni ya Urais kwa tiketi ya CCM iliyofanyika Iringa Mjini ambapo ameeleza namna ambavyo Serikali ya CCM ilivyotekeleza mradi wa maji wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 41 utakaowezesha wananchi wa Mafinga Kaskazini kupata maji kwenye mabomba.

“Mhe. Rais miradi mingi ya maji uliyotuletea ya zaidi ya shilingi bilioni 43 ilikuwa ni ya kuchimba visima, ila sasa tunaenda kutandika mabomba katika kata nne za jimbo la Mufindi Kaskani,” Mhe. Kigahe amesema.

Katika sekta ya Elimu, amesema Serikali ya Awamu ya Sita, imetoa kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 2.4 ambazo ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa ya viwango vya juu.

Wakati unaingia madarakani, kata moja katika jimbo la Mufindi Kaskazini ilikuwa haina umeme, ila ndani ya miaka minne na nusu umetuletea huduma ya umeme na kuweka historia.

Mhe. Kigahe, amesema kuwa Rais Samia ametekeleza mengi ndani ya miaka minne na nusu tangu alipoingia madarakani ambapo katika sekta ya miundombinu, jimbo hilo liliomba ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya kilomita 10 na kupewa barabara yenye urefu wa kilomita 32 za kiwango cha lami.





TABASAMU LA KWELI KUTOKA KWA RAIS DKT. SAMIA

Ni mtu wa watu, mchapakazi na muadilifu, mwenye roho ya upendo waswahili tunasema roho nyeupeeee yani kiroho safi, hana makuu na mpenda haki ambaye nyakati zote ametanguliza Utu katika utendaji wa majukumu yake.

Huyu ni Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Oktoba 29, Mpe Kura Yako



ROSE AMPONGEZA RAIS SAMIA KUHUSU BIMA YA AFYA KWA WASIOJIWEZA

Mbunge wa viti maalumu mteule mkoa wa Iringa kupitia Chama Cha Mapinduzi Rose Tweve, amempongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, mgombea Urais kupitia chama hicho, kwa ahadi yake kuwa atahakikisha wasiojiweza watapata Bima ya Afya, hii itamfanya kuingia katika kitabu cha historia cha watanzania.

Rose ametoa pongezi hizo katika Mkutano wa Kampeni ya Mgombea Urais iliyofanyika Iringa Mjini leo Septemba 7, 2025.

"Katika kampeni zako umeahidi kwamba ndani ya siku 100, watu masikini watapata Bima ya Afya na hii itafanya kuingia katika historia ya kitabu cha watanzania kwa kujali utu wa wananchi wako. Unaenda kuweka alama kwenye mioyo ya watoto ambao wangekatisha ndoto ya maisha yao kwa kuwa wazazi wao walishindwa kumudu huduma za matibabu." Alisema Rose.





KONA YA ILANI

Kukuza na Kuimarisha
Matumizi ya Sayansi na
Teknolojia katika Shughuli
za Kiuchumi na Kijamii.



DKT. SAMIA ATANGAZA NEEMA JIMBO LA MVUMI

Mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema iwapo atapata ridhaa ya kuchaguliwa tena, Serikali yake itatekeleza ujenzi wa miradi ya barabara, ujenzi wa madarasa, na kuleta maji safi na salama kwa wananchi wa jimbo la Mvumi.

Mhe. Samia, amesema hayo leo kwenye mkutano wa kampeni za Uchaguzi Mkuu za CCM, Jimbo la Mvumi, Mkoa wa Dodoma.

Akiongea na umati wa watu uliojitokeza kwenye Mkutano wa Uchaguzi Mkuu kwa mgombea Urais CCM, uliofanyika jimbo la Mvumi, Mhe. Samia, ameahidi kutekeleza ujenzi wa barabara inayohudumia kata 17 ya Makangwa-Mlowa-hospitali ya wilaya yenye urefu wa kilomita 18 iliyoombwa na mbunge wa jimbo hilo Job Lusinde.

“Nimepokea maombi matatu ya mbunge wenu na tutaangalia namna ya kuyatekeleza,” Mhe. Samia amesema.

Kwenye maeneo yanayo pata maji ya chumvi katika vijiji vitatu alivyoomba mbunge wenu Lusinde nimelichukua na tutaona nini cha kufanya,” Mhe. Samia ameahidi.

Kuhusu ombi la ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita, Mhe. Samia, ameahidi kulitekeleza nakuongeza kuwa Serikali yake inafahamu uwepo wa kata tatu zenye uhitaji wa madarasa na itazitekeleza.



#ATATEKELEZA





KUTOBA



KUFAKILI



*Kazi na Utu
Tunasonga Mbele*

ssh_anatekeleza